



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA



TAREHE: 30/09/2024

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(limetolewa kwa kuzingatia kanuni ya 7(1)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa anawatangazia wananchi wote uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake Vijana na Watu wenye Ulemavu ambapo jumla ya Tshs. **859,435,653/=** ambapo Wanawake **Tshs. 343,774,261/=** Vijana **Tshs. 343,774,261/=** na Watu wenye Ulemavu **Tshs. 171,887,130/=** zimetengwa kwa robo ya pili ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, hivyo vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za Serikali za Mitaa iliyopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mkopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- i. Kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi wa Halmashauri.
- ii. Kikundi kiwe kinacho jishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.
- iii. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanavikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha Watu wenye Ulemavu kiwe na wanavikundi wasiopungua wawili (2), pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) Mtu mwenye Ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha Watu wenye Ulemavu iwapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa

Mtu mwingine mwenye Ulemavu wa kuungana nae katika eneo lake. Aidha, sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.

- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa na jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali: na
- v. Wanakundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyne akili timamu na wenyne umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha kikundi cha vijana kinapaswa kiwe na wanavikundi wenyne umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmsahauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mikopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinatakiwa kuwa na viambatanisho vifuatavyo:- barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Mtendaji wa Mtaa, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unao ombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyondani ya mfumo na taarifa ya Akaunti ya Benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 25 Oktoba 2024

Tangazo limetolewa na :-


**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
Kastori G. Msigala IRINGA**

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI
MANISPAA YA IRINGA**